# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# OFISI YA WAZIRI MKUU- TAMISEMI

# HALMASHAURI YA MJI WA MBULU

# SHULE YA SEKONDARI GUNYODA

S. L. P 18,
Mbulu Manyara – Tanzania
Tarehe………………….

**Mkuu wa Shule – 0787 043 704**
**Makamu Mkuu wa Shule- 0620 470 280**
**Mwaka:…………………….**

Mzazi/ Mlezi wa
Mwanafunzi,…………………………………………………………………………

S.L.P,…………………………………………………………………………………

**Yah: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI GUNYODA, HALMASHAURI YA MJI WA MBULU, MKOA WA MANYARA, MWAKA……………**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka …………..


Shule ya Sekondari GUNYODA ipo umbali wa Kilometa 12 Kaskazini Magharibi mwa Mji wa MBULU. Usafiri wa Daladala kutoka mjini MBULU unapatikana katika kituo cha mabasi MBULU MJI. Nauli ni Shilingi 2,000 kwa Daladala na Pikipiki ni Shilingi 5,000.

Mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe…………….. Mwisho wa kuripoti ni tarehe…………….


**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:**

**A. Sare za Shule (Kwa wasichana)**

i. Sketi rangi ya CHUNGWA (RED ORANGE) pea mbili. Utajishonea, yenye marinda kumi na mbili 12. Urefu wa sentimita 30 kutoka kwenye magoti kuelekea chini. (rangi ni kama inavyoonekana hapo chini)




ii. Shati nyeupe yenye mikono mirefu pea mbili-Utajishonea / kujinunulia.
iii. Tai ndefu yenye rangi ya CHUNGWA (RED ORANGE).
iv. Soksi jozi mbili nyeupe za shule.
v. Sweta 1 rangi ya ZAMBARAU ILIYOKOLEA (DARK PURPLE) ya shingo V. (rangi ni kama inavyoonekana hapo chini)




vi. T-Shirt ataikuta shuleni (Aje na shilingi elfu kumi na tano kwa ajili ya T-Shirt). Kwa anae hitaji kununulia shuleni
vii. Kwa Waislam tu waje na Hijab (kijuba) iwe nyeupe ifunike kifua cha mwanafunzi
viii. Sare za michezo: Track suti rangi ya Bluu, tisheti 1 ya njano shingo duara na raba.
ix. Viatu vya shule pea mbili ni vyeusi vya kufunga na kamba.
x. Traksuti nyeusi kwa ajili ya kuvaa usiku.
xi. Sketi ya kazi rangi NYEUSI ndefu sentimita 30 kutoka kwenye magoti kuelekea chini

**3. Mahitaji mengine muhimu:**

- Madaftari 10 (Q4), kalamu, Rula, mathematical set, Scientific calculator, Ream Mbili (A4) kwa mwaka.
- Mwanafunzi wa PCB aje na Dissecting kit.
- Vitabu vya ziada na kiada kama ifuatavyo;
    - PHYSICS – S. CHAND ONE, S. CHAND TWO
    - CHEMISTRY- NGAIZA SERIES-PHYSICAL CHEMISTRY, ORGANIC CHEMISTRY, GENERAL CHEMISTRY AND INORGANIC CHEMISTRY
    - BIOLOGY- S. CHAND AND BIOLOGICAL SCIENCE (BS)
- Barua ya maagizo (Joining instruction).
- Vivuli vya vyeti vya Kidato cha Nne, Leaving Certificate na Cheti cha Kuzaliwa.
- Medical Examination Certificate kutoka Hospitali ya Serikali.
- Mto 1, foronya 2 (pink na blue), Mashuka jozi 2 (pink na blue), blanket, chandarua.

- Mwavuli, Rain boots fupi nyeusi.
- Godoro inch 3 (futi 2.5).
- Vyombo: Sahani ya bati (Aluminium), kikombe, bakuli, kijiko.
- Sanduku la bati/chuma lenye kufuli.
- Bima ya Afya au aje na TSH 50,400 shuleni kwa asiye na bima ya afya
- Ndoo 3 (lita 10) zenye mifuniko.
- Vifaa vya usafi: Jembe, Brashi ya chooni, na mopa ya kudekia.

**4. Michango mbalimbali**

| Na. | Aina ya Mchango | Kiasi (TSH) |
|---|---|---|
| 1 | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 2 | Tahadhari | 5,000/= |
| 3 | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| 4 | Nembo ya Shule | 5,000/= |
| | **JUMLA** | **80,000/=** |

**Malipo yafanyike Benki ya NMB: Ac.No. 41210020173 (GUNYODA SECONDARY SCHOOL DEVELOPMENT ACCOUNT)**

**5. Sheria na Kanuni muhimu za Shule**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yamefafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

**5.1 Sheria na Kanuni za Shule**

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule.
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (Preparation).
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa.
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.

vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
ix. Kutunza mali za shule.
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari, na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**5.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi.
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro.
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo.
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule.
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule.
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya.
viii. Uvutaji wa sigara.
ix. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa.
x. Kupata ujauzito au kutoa mimba.
xi. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
xii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni.

xiii. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
xiv. Kudharau Bendera ya Taifa.
xv. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu, na
xvi. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

.

# MEDICAL EXAMINATION FORM

To be completed by Medical Officer from a known Public Hospital or Health Centre in respect to all entrants

Full name……………………..……………..Age……...Sex…………year…..

1. Blood count (Red and White) ………………………………………...
2. Urinalysis Test ……………………………………………………….
3. Syphilis test……………………………………………………………
4. T.B.……………………………………………………………………………
5. Eye Test …………………………………………………………………
6. Ears…………………………………………………………………………
7. Spleen………………………………………………………………………
8. Abdomen ……………………………………………………………….

ADDITIONAL INFORMATION: e.g. Physical impairment, family disease, chronic infections etc.

…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………

I certify that the above named individual is fit to pursue studies as stated above.

Name …………………………….. Designation …………………………..

Signature ..………………………. Station; ………………………………

Date ……………………………. Official stamp

**NOTE:**

1. Medical officer during the course of this Examination please attend the individual according to any diagnosed case.
2. The dully filled form must be handed to the Head of the School during registration week, under No circumstances should a student be registered without certification of his/her physical fitness.

**Thank you in Advance**

**………………………**

**HEADMASTER**
**GUNYODA SECONDARY SCHOOL**

## AHADI YA MWANAFUNZI

Mimi mwanafunzi ………………………………………………wa kidato cha Tano chaguo ……………………….. (Tahasusi) mwaka wa masomo…………..
Ninakiri kusoma, kuelewa na kuahidi kutii taratibu zote zilizoainishwa katika fomu iliyotumwa kwangu na Mkuu wa shule ya Sekondari Gunyoda.
Nitatoa ushirikiano wa kutosha kwa walimu wangu na shule kwa ujumla katika muda wangu wote nitakaokuwa shuleni, ili niweze kupata elimu na kuendeleza jamii na Taifa langu.
Ninaahidi na kukiri kuwa sintashiriki kwenye mgomo kwa namna yoyote ile.

Jina:…………………………………. Saini ………………. Tarehe……………….

## AHADI YA MZAZI / MLEZI

Mimi ………………………………..wa S.L.P……… Mji …………Simu ……………

Ambaye kazi yangu ni …………………………………. natamka hapa kama mzazi / mlezi wa ……………………………………………………………………………

Ninakubali kwa hiari yangu mwanangu asome katika Shule ya Sekondari Gunyoda kuanzia tarehe ………………………………..

Ninaahidi kama ifuatavyo:-

1. Kwamba nimekubali chaguo alilopewa mwanangu na sitamruhusu kubadilisha hadi apate kibali cha maandishi kutoka kwa mamlaka husika.
2. Ninaahidi kumpatia mwanangu vifaa vyote kama vilivyoainishwa katika fomu ya kujiunga ikiwemo SARE KAMILI ya shule bila kuharibu chochote.
3. Ninatambua ya kuwa walimu wanahitaji ushirikiano wangu katika kumpatia mwanangu elimu na nitashirikiana nao bega kwa bega kwa masuala yanayomhusu mwanangu kitaaluma na nidhamu ili aweze kufikia malengo yake na ya Taifa.
4. Naahidi kuwa endapo mwanangu ataenda kinyume na taratibu zilizoainishwa katika fomu hii achukuliwe hatua stahili za kinidhamu kama alivyoorodheshewa.

Jina: …………………………………. Saini…………… Tarehe…………………

Uhusiano na mwanafunzi: ……………………………………………………………

## 6. Viambatisho na Fomu Muhimu

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali,
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai,
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule, na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**NB:** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**ANGALIZO: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa Shule: 0787043704**
- **Makamu Mkuu wa Shule: 0620 470 280**

Mwisho Kwa niaba ya jumuiya ya GUNYODA Sekondari napenda kukukaribisha shuleni, kukutakia safari njema na

mafanikio mema katika masomo yako ya kidato cha tano na sita.

**"KARIBU SANA GUNYODA SEKONDARI"**

**Saini ya Mkuu wa Shule ……………………**

**Jina la Mkuu wa Shule…………………….**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule**